

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam,
28 Aprili, 2005

Kumb. Na: EA 45/257/01/134

**WARAKA WA UTUMISHI NA: 4 WA MWAKA 2005 KUHUSU
MAFUNZO ELEKEZI YA AWALI KWA WATUMISHI WA UMMA
(ORIENTATION COURSE)**

1. Utangulizi

Kufuatia kutungwa kwa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998 Serikali ilipitisha Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo. Malengo ya Sera hiyo ni pamoja na kuimarisha nidhamu, ufanisi, uadilifu, ustahifu, uwezo na utendaji bora wa kazi katika Utumishi wa Umma, kwa kusisitiza mwelekeo na misingi ya Sheria na taratibu, ili kuleta mabadiliko ya kweli kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Ili malengo hayo yafikiwe, hapana budi pia kuwapatia watumishi maarifa na nyenzo muhimu za kazi pamoja na mafunzo yanayotolewa kazini. Hivyo, imeonekana kuwa kuna umuhimu kwa Serikali kuyapa msukumo mpya mafunzo ya awali (induction training) kwa watumishi wote wapya wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma, ili waweze kujua wajibu wao, na pia kuufahamu utamaduni wa utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

2. Madhumuni ya Waraka huu

Madhumuni ya Waraka huu ni kutoa mwongozo unaoelekeza wajibu na umuhimu wa Wizara na Idara za Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wote wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wanapatiwa mafunzo ya utendaji na uendeshaji kazi Serikalini yaani, mafunzo elekezi (Public Service Orientation Course).

3. Agizo

Kwa Waraka huu waajiri wote wanaagizwa kuhakikisha kuwa watumishi wao wote wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wanapatiwa mafunzo hayo ndani ya kipindi cha miezi sita tangu mhusika aajiriwe. Aidha, waajiri wote wahakikishe watumishi hao wanafanyiwa upekuzi kama sehemu ya mafunzo hayo. Waajiri wanakumbushwa tena wahakikishe kuwa kila wanapopanga bajeti za Wizara / Idara zao suala la bajeti kwa ajili ya mafunzo hayo kwa watumishi wapya au ambao hawajahudhuria mafunzo hayo linazingatiwa ipasavyo.

4. Hatua za Utekelezaji

- 4.1 Mafunzo haya yatasimamiwa na Chuo cha Utumishi wa Umma - Magogoni. Hata hivyo, kwa vile Ibara ya 2 ya Sera ya Menejimenti na Ajira inasisitiza umuhimu kwa waajiri kutoa mafunzo kwa watumishi, gharama za mafunzo zitatolewa na waajiri wenyewe kupitia bajeti zao.
- 4.2 Mafunzo haya yatatolewa mara mbili kila mwaka ili kuhakikisha kuwa watumishi wapya wanapewa mafunzo haya kabla ya kuanza kazi.
- 4.3 Inasisitizwa kuwa mafunzo yanawahusu watumishi wa taaluma zote na yanalenga kuwaelekeza wahusika kuhusu taratibu za uendeshaji kazi Serikali. Hivyo basi, watumishi wa kada zote katika Utumishi wa Umma watalazimika kupitia mafunzo hayo.

5. Mwisho

Waraka huu unaanza kutumika tarehe 01 Mei, 2005.

Joseph A.M. Rugumyambeto
KATIBU MKUU (UTUMISHI)